SHELL ILIVYOWATOA, KUWATUMIA WANAJIOLOJIA WATANZANIA

Ephrahim Bahemu, Mwananchi
ebahemu@mwananchi.co.tz

Mtoto anapozaliwa huanza kukua na baada ya muda fulani hupata utambuzi unaomsababishia matamanio ya vitu na kujenga ndoto zake.

Si watu wote ambao hufanikiwa kutimiza ndoto hizo lakini wengine hutimiza ingawa si kwa wakati waliotegemea.

Sababu za yote hayo zipo nyingi kwa kuwa kila mtu atatoa ya kwake.

Wapo wanaofanikiwa kwa kupambana hadi mwisho na kuna wengine wanashikwa mkono kutimiza ndoto zao.

Hata hivyo, wakati mwingine ndoto inaweza kubadilishwa kutokana na mazingira na watu wanaokuzunguka, mabadiliko yanaweza kuwa chanya au hasi.

Catherine Mushi muda wote ndoto yake ilikuwa ni kuhudumia sekta ya usafiri wa anga kama rubani lakini hajafanikiwa kutimiza hilo.

Kwa sasa Mushi ni mwanajiolojia na anafanya kazi katika Kampuni ya Mafuta na Gesi ya Shell, japo si rubani kama ilivyo ndoto yake lakini yupo kama 'rubani' akizungukia miradi mbalimbali ya Shell nje ya Tanzania.

"Ndoto yangu ya utotoni ilikuwa ni kuwa rubani wa ndege, lakini matamanio yalikuwa si kazi ya urubani bali kufanya safari za anga na kupata fursa ya kusafiri ndani ya Tanzania na ulimwengu mzima. Siwapeleki watu mapumziko kama ilivyokuwa ndoto yangu bali nachunguza mahali palipo na nishati ya kuwapatia," anasema Mushi.

Pia, anasema hamasa ya kufanya anachokifanya sasa ilitoka kwa mama yake (amefariki dunia) ambaye alimsisitiza umakini na kujituma katika shughuli zake, hivyo alisoma kwa bidii na kufanikiwa kuhitimu shahada yake ya jiolojia katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mara baada ya kuhitimu shahada yake ya kwanza, ilijitokeza fursa kwa vijana waliomaliza chuo, hiyo ilikuwa ni mwaka 2014 na fursa hiyo ilitangazwa na Shell ambayo wakati huo ilikuwa ikiitwa BG Group.

Mwanajiolojia Catherine Mushi anayefanya kazi katika Kampuni ya Mafuta na Gesi ya Shell. **Picha na Mpigapicha Wetu**

"Kama ilivyo kwa watu wengi fursa niliyoipata ilikuwa ya manufaa sana, kwa kuwa nilipata kufanya kazi katika mataifa na watu tofauti wenye historia tofauti, Nikiwa kama kijana mdogo kujiunga na kampuni hiyo nikitokea chuo moja kwa moja ilikuwa ni changamoto.

"Nilipaswa kujifunza haraka na kubadilika kulingana na mazingira, nilipaswa kuwasilisha matokeo ya mradi lakini nilikuwa nikipewa ushirikiano na motisha kutoka kwa mameneja na wafanyakazi wenzangu," anasema Mushi.

Pia, anasema ujuzi alioupata kutoka kwa wataalamu wa kimataifa aliokutana nao kufanya kazi ni muhimu sana katika maisha yake na imani yake ni kuwa sekta ya mafuta na gesi ina nafasi kubwa katika maendeleo ya Tanzania, Uganda na Msumbiji.

Mwingine ni Frank Marealle aliyepata fursa kuendelezwa kitaaluma na Shell na sasa ni mhandisi wa jiolojia katika kampuni hiyo kubwa ya mafuta na gesi duniani.

Marealle ambaye ana shahada ya uzamili ya uhandisi wa kemikali alianza kufanya kazi Shell (iliyokuwa BG Group) mwaka 2013 kupitia mpango wa kimataifa wa kampuni hiyo kwa wahitimu ambao walikuwa wakipatiwa mafunzo ya miaka miwili.

Anasema kupitia mpango huo alianza kwa kufanya kazi hapa nchini kisha akapelekwa Australia na baadaye India kisha akafanya mtihani wa ithibati ili kukidhi vigezo vya kuwa mhandisi ambaye anaweza kufanya kazi mahali popote duniani.

"Niilifurahi sana kuwa kwenye kampuni kubwa inayoongoza katika sekta.

2014

Mwaka ambao Shell ilikuwa inaitwa BG Group.

"Vitu vingi vilikuwa vinapatikana kwenye meli, mkchezo na mambo mengine, shifti ilikuwa ya saa 12; na kazi ilikuwa ni kuchoronga."

Oscar Mmari

Hii ilikuwa ni fursa kubwa kwangu kuungana na timu ya wataalamu wa viwango vya dunia. Shell wana viwango vyao kwa wafanyakazi wote ambavyo ni vya juu sana na mafunzo yanatolewa kwa wote," anasema Marealle.

Anasema hivi sasa yeye ni mtaalamu ambaye anaweza kushindana duniani kote na kutokana na uzoefu wake anayaona mafanikio mbele katika mradi wa gesi asili iliyosindikwa (LNG) huko mkoani Lindi na yupo tayari kutoa mchango wake kufanikisha hilo.

Oscar Mmari ni miongoni mwa wanajiolojia vijana wa Kitanzania ambao Shell imewatoa, yeye alijiunga na kampuni hiyo mwaka 2014 ambao vijana kutoka maeneo tofauti duniani walifanyiwa mafunzo ya shughuli za mafuta na gesi kwa miaka miwili.

Mmari anasema uzoefu alioupata umemuongezea uwezo wake wa kuhudumu katika sekta hiyo hususani uzoefu wake wakati wa utafiti wa gesi ya Kamba-1, Mtwara ambao muda mwingi yeye na timu yake walikuwa wakiutumia kwenye meli ya kisasa na helikopta kwa kuwa mradi ulikuwa wa katikati ya bahari.

"Vitu vingi vilikuwa vinapatikana kwenye meli, michezo na mambo mengine, shifti ilikuwa ya saa 12; na kazi ilikuwa ni kuchoronga. Nilijifunza mambo mengi ya mazingira na kibalolojia na mimi kazi yangu ilikuwa ni kuelekeza mahali pa kuchoronga kwa kuzingatia tathimini za kitaalamu," anasema.

Kwa sasa Mmari anajiandaa kufungua ukurasa mpya wa maisha ya taaluma yake kwa kwenda Houston, Marekani kwa ajili ya majukumu mapya ya Shell.

Asimwe Ruganyoisa ambaye elimu yake ni shahada ya uzamili katika uhandisi wa mafuta ni miongoni mwa wanufaika wa mpango wa Shell wa kuwaendeleza vijana wanaochipukia kwa kuwapa mafunzo na uzoefu wa sekta.

Anasema wakati wa programu hiyo alikuwa aksafiri na kufanya kazi katika nchi za Bolivia, Russia, Marekani na Uholanzi na sasa anaiona nuru ya kesho yake katika sekta hiyo na taaluma yake.

"Jambo lililonivutia kujiunga na programu hiyo ni kwamba unapomaliza lazima upate walau miaka ya kufanya kazi ili kupata uzoefu na wakati nikiwa naendelea na programu ndipo BG iliunganishwa na Shell na hapo kampuni ikawa kubwa zaidi," anasema Ruganyoisa.

Pia, anasema kwa sasa anakusudia kutumia uzoefu wake alioupata kwa kuongeza thamani katika miradi ya LNG Tanzania, "muda ambao nimefanya kazi katika kampuni hii ni mzuri sana nilipata uzoefu muhimu unaonikuza katika taaluma yangu."